


# Jarida la UQAB

Toleo 41 - Shawwal 1441 H / Juni 2020 M





# UFADHILI WA IMF COVID -19 NI CHOMBO CHA KUOKOA UKOLONI WA KIUCHUMI WA NCHI ZA KIMAGHARIBI

## UFADHILI WA IMF COVID 19 NI CHOMBO CHA KUOKOA UKOLONI WA KIUCHUMI WA NCHI ZA KIMAGHARIBI





Hadi kufikia sasa , Shirika la kifedha la kimataifa IMF limeidhinisha jumla ya bilioni kumi na nane dolari ($18 dolari) kwa minajili ya kusaidia nchi kadhaa ili kuhimili maafa ya janga la korona. " Tangu mwanzoni mwa Aprili hadi May tarehe sita, jana, tumeidhinisha ufadhili wa kifedha uliopo chini ya mpango waa kidharura kwa nchi 50 ." alisema Gery Rice, mkuu wa Idara ya mawasiliano ya IMF katika mkutano halisi na vyombo vya habari. " Ni IMF inasonga kwa kasi isiyo ya kawaida kwa njia isiyo ya kawaida ili kutosheleza hitajio lisilo lakawaida ambalo leo soteni tuna likabili."

Alisema zaidi ya nchi mia moja zilikuwa zimepeana mapendekezo ya kutaka usaidizi kutoka IMF tangu kuanza janga la COVID 19. Msemaji kisha aliendelea kusema kuwa shirika hilo lilikuwa limeongeza fursa ya kupata mkopo kwa mipango yake ya kidharura-RCF na RFI, ilikukidhi haja ya kiulimwengu ya dolari bilioni mia moja($100). Bwana Rice alifafanua kuwa usaidizi wa dharura wa Covid 19 ulikuwa haufananishwi na mipango ya kawaida ya IMF kwani mpango huo haukuwa umefungamanishwa na masharti yeyote.

"La muhimu, ni kuwa mipango hii inaruhusu shirika kupeana usaidizi wa kidharura bila kuhitajia mpango mzima kamilifu. Kwa hio hauhitaji masharti ya kawaida ya IMF." Alisema bwana Rice. Kuhakikisha hakuna matumizi mabaya ya fedha hizo, Rice alisema kuwa nchi shirika waliombwa kutoa hakikisha ya kwamba fedha hizo zitatumiwa tu kwa minajili ya yale yanayo husiana na Covid 19.{Anadolu Agency}

Usaidizi huu mkubwa wa IMF kwa janga la Korona unadhihirisha wazi jinsi namna gani shirika hili moja pekee lilivyo na fedha zakutosha kusaidia uchumi wa kiulimwengu. Isitoshe mkuu wa IMF Bi. Kristalina Georgieva aliongezea kwa kusema kuwa Shirika lake liko tayari kutumia kwa ukamilifu dolari trilioni moja ambayo ingalipo katika hazina yake ilhali viongozi wa kimagharibi wameita mwito kwa IMF kuzidishiwa ufadhili zaidi.




Ama swali lakuulizwa ni vipi usaidizi huu wa fedha wapatikana kwa sasa lakini haupatikani nyakati zengine kusaidia nchi za ulimwengu wa tatu kupambana na umasikini, kuboresha hali ya afya na elimu, vyakula au kusaidia asilimia kumi ya watu ulimwenguni ambao World bank dadake IMF yasema kuwa wanaishi chini ya umasikini? Jawabu kwa hili ni kuwa IMF na World Bank zilibuniwa si kwa minajili ya kusaidia hali za walimwengu bali ni kumakinisha nidhamu ya kikoloni ambayo inasaidia uchumi za kimagharibi.

Kabla ya vita vya kiulimwengu vya pili,nchi za bara Uropa zilibuni tawala pana za kifalme ambazo kutokana kwayo zilikuwa zikinyonya rasilimali na nguvu kazi, huku zikiwauzia machine na mitambo ya kimagharibi kwa bei za juu mno hadi ulipaji wake ukawa unazalisha ufifiaji wa mali wa nchi tawaliwa. Ni kwa muundo huu ndio umekuwa ukiendelezwa kiulimwengu baada ya kumalizika kwa ukoloni asili, kwa nchi za kimagharibi zikiendelea kupora mali, raslimali na nguvu kazi za nchi zengine ulimwenguni.

Ama malengo ya IMF na World Bank, zilizobuniwa mwaka wa 1944 kama badala ya nidhamu koloni ya kiuchumi ya tawala ya koloni asili, ni kumakinisha kolono mpya mambo leo..Kwa mda, ufifiaji wa wingi wa mali husababisha ukosefu wa amani ya kiuchumi ndani ya nchi. Malengo ya IMF kwa hili huwa ni la kisiasa zaidi kuliko la kiuchumi: IMF huingilia kati pindi amani ndani ya nchi imekuwa haiangaliliki kisiasa, basi huwa ndio ni yenye kupeana ufadhili wa kifedha wa haraka kwa serikali iliodhaifu kisiasa. Na kupitia masharti yaliofungamanishwa na mikopo hiyo, IMF huhakikisha uendelezaji wa utabikishaji wa nidhamu ya kiuchumi ya kirasilimali kwa nchi hizo na hulazimisha sera maalum ju yao ambazo huhakikisha uendelezaji wa nchi hizi kuzidi kuporwa na kunyanyaswa.Na hii hujumuisha kupendekeza usafirishaji, kuruhusu mtiririko wa mtaji wa kifedha za kimataifa, na kuelekeza matumizi ya kifedha katika ujenzi unaofaidisha biashara ya kimataifa badala ya ujenzi unaofaidi uchumi wa ndani ya nchi.




Ama wamagharibi utegemeaji wao wa uchumi wa kikoloni ni kwasababu ya wao kutabikisha nidhamu ilio feli ya kiuchumi ya kirasilimali. Nidhamu hii awali huzalisha kwa wingi amali za kiuchumi lakini baada ya mda hupunguza uzalishaji wa kiuchumi kwani matajiri wakubwa wachache hukuwa kwa gharama ya wengi ya watu.

Hawa matajiri wachache hawawezi kuzalisha kiwango cha kiuchumi kinachohitajika kukidhi haja ya idadi kubwa ya watu hivyo basi kulazimika kutazama nje ya nchi. Hali ya nchi za kimagharibi sasa ni kuwa ni zenye kutegemea kwa wingi bidhaa za kiviwanda kutoka nje.

Islam ulitabikishwa zaidi ya miaka elfu moja, na kupitia kipindi hiki, ulijenga uchumi uliokuwa wa nguvu na jasiri ulioendelezwa kiukweli na amali za ndani za nguvu za kiuchumi. Kwa uhakika uchumi chini ya uisilamu uliuongoza ulimwengu na ndio sababu kuu ya kukuwa kwa biladi za magharibi kabla ya wao kukumbatia ukoloni kwani nchi za kimagharibi zilikuwa zategemea mno biashara na biladi za kiisilamu. Allah swt asema katika Quran tukufu

[هُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ ذَلُولًا فَامْشُوا فِي
مَنَاكِبِهَا وَكُلُوا مِن رِّزْقِهِ وَإِلَيْهِ النُّشُورُ]

**“Yeye ndie aliyeidhalilisha ardhi kwa faida yenu –basi tembeeni katika pande zake na kuleni katika riziki zake, na kwake yeye ndio kufufuliwa.” [al-Mulk: 15]**

Kwa kudra za Mwenyezi Mungu {SWA}, ulimwengu karibuni utaona kurudi kwa dola la Khilafah kwa njia ya Mtume [SAW} ambayo itakayo unganisha biladi za waisilamu chini ya uwongozi wake, utakataa uingililiaji kati wa mataifa ya kigeni, utatabikisha Sheria za Kiisilamu naujenge tena ustaarabu uongozao ulimwenguni ambao utakuwa ndio chimbuko la amani na maendeleo kwa wanaadamu wote.

**Faiq Naja**

# SERIKALI KUONGEZA HOFU NYENGINE YA NJAA BAADA YA ILE YA VIRUSI VYA KORONA!




Kama hatua yake mpya ya kukabiliana na janga la kiulimwengu la Virusi vya Korona, serikali imeamua kuyafunga maeneo mawili yenye idadi kubwa ya Waislamu ambayo pia ni vituo muhimu vya kibiashara; Eastleigh Jijini Nairobi na Old Town, Mombasa. Madai ya Serikali kuwa hatua hio haikuchukuliwa kwa nia ya kuadhibu wakaazi wake, bali ni kwa malengo ya kulinda maisha ya wakenya dhidi ya maambukizi, kwa kuwa maeneo hayo yamerekodi visa vingi vya Covid-19.

Hatua hii itaendeleza zaidi hali mbaya ya kiuchumi hasa ikizingatiwa kwamba maeneo hayo hutumiwa na watu wengi katika kuendesha biashara kama njia ya kuweza kukimu mahitaji yao kila siku. Hatua ya kuweka vikosi vikubwa vya polisi inaonyesha wazi kwamba marufuku hiyo ya kuzuia kuingia na kutoka maeneo hayo kwa siku kumi na tano, ni kuwaadhibu na kuwanyanyasa wakaazi wake kiuchumi. Ni bayana kwamba serikali imeamua kuongeza hofu nyengine ya njaa kwa raia wake baada ya ile ya maradhi ya Korona. Cha kutamausha ni kwamba vikosi vya usalama vinavyo hakikisha marufuku hiyo inatekelezwa, havikuonekana pindi magenge ya vijana yalipokuwa yakitekeleza uhalifu dhidi ya wakaazi wa Old Town. Na huku serikali ikidai kuwa hatua yake hiyo ni kujali maisha ya raia wake, maajabu serikali imepuuza raia wengine walioachwa bila makao kwa sababu ya mafuriko! Linalo huzunisha ni kuwa tokea msimu wa mvua za masika kuanza hadi sasa mafuriko tayari yameua zaidi ya raia 100!

Tunasema kuwa, dola za kirasilimali huyapa kipaumbele mapato ya kiuchumi juu ya maswala ya kiafya, wakuu wa serikali ya

Kenya waliruhusu ndege kutoka China kutua humu nchini baada ya mkurupuko wa maradhi ya Korona huko China. Na sasa kinacho onekana ni kwamba



serikali inacheza mchezo wa kuwatupia lawama raia wake ilhali iliruhusu virusi hivyo kuingia nchini.

Kimsingi, suala upimaji maradhi hayo ni jambo zuri, ila hatua ya raia kususia zoezi hili inamaanisha kwamba hawana imani na viongozi ambao wamekuwa na mazoea ya kuhadaa raia kila siku. Mifumo duni ya kiafya na takriban huduma zote za kijamii yote haya yamewafanya raia kutokuwa na imani na Serikali. Tayari kuna ripoti kwenye baadhi ya vyombo vya habari zinazo onesha watu wakitoroka vituo vya karantini za serikali viko katika hali mbaya na wengine kutishia kujitoa uhai wao kwa sababu ya shida wanazo kumbana nazo.

Kwa ujumla, maambukizi haya ya virusi vya Korona yametuonyesha kwamba umma sio tu nchini Kenya bali ulimwengu kwa jumla umekosa usimamizi wa kikweli wa mambo yao. Na kwamba viongozi wa kisekula kote duniani huwabwagia lawama na kuwatisha raia wao kama njia mojawapo ya kujaribu kuficha utepetevu wao wa kila mara. Hivyo kuna haja kubwa sana ya umma kote duniani kufanya kazi na Hizb ut-Tahrir kuleta uongozi unaojali kweli maisha ya watu sio kwa misemo tu bali kwa vitendo. Uongozi huo sio mwengine bali ni Khilafah ambao kiongozi wake hatochukulia utawala kama chombo cha kunyanyasa raia wake kwani atafahamu kwamba kuna siku ataletwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mfalme wa wafalme ahesabiwe jinsi gani alivyo endesha uongozi wake. Serikali hiyo ni Khilafah kwa njia ya Utume ambayo kikweli raia ndio watakuwa na imani nayo.

**Shabani Mwalimu**

# YANAYOWAKUMBA UMMAH NI MABAYA MARA NYINGI ZAIDI KWA WANAADAMU WENGINE



Mwanaadamu ni kiumbe, cha kibinafsi na pia ni kiumbe cha kijamii, kiasi cha kuwa balaa la kibinafsi na la kijamii humuathiri. Quran inaeleza kuwa mwanaadamu atatahiniwa na majanga kama uzee, maumivu, kiu, njaa, machofu, hofu, kupotea kwa mali, maisha na vitu. Kuna kuwepo pia maafa katika Dini, nayo ni kuwacha njia ya Dini na kuvunja amri za Mwenyezi Mungu na mipaka. Kwa mfano, kuyumba katika masuala ya imani ni balaa kubwa katika Dini. Kutotekeleza swala, kutokufunga, riba, kusengenya na kudanganya yote ni balaa katika Dini. Hadi hapa, yote hiyo ni mifano ya maafa katika kiwango cha kibinafsi. Pamoja na haya, kuna maafa katika kiwango cha kijamii, ambayo humuathiri kila mtu katika jamii, wale waliofeli na wale wasio na hatia, kwa namna ile ile. Fikra yoyote inayodhuru kiini cha Uislamu, ambayo inawavuta watu nje ya Uislamu ni maafa. Wanazuoni, wanaoshindwa kuzungumza haki; watawala, wasiotawala kwa Uislamu, ni maafa. Kutotekeleza Uislamu kimfumo, makafiri kuwa na nguvu na satwa juu ya Waislamu, huku wakipiga marufuku mfumo wa Kiislamu na kuufanya historia, yote ni katika maafa. Kutofahamu maafa haya, au kufahamu bila kuyakanusha, ni aina ya

[أَيْدِيكُمْ بَتْ◌َكَس فَبِمَا مُّصِيبَةٍ مِّن أَصَابَكُم وَمَا]

**“Na misiba inayo kusibuni ni kwa sababu ya vitendo vya mikono yenu.” (Ash-Shuraa: 30)**

Maafa katika kiwango cha kijamii daima yamepelekwa kwa mataifa kutokana na madhambi yao, uasi wao; kwa kukanusha, na kuwadhulumu Mitume wao na wale wanaowaunga mkono Mitume. Aina hii ya maafa muda wote imepelekea katika maangamizi ya taifa hilo. Mataifa ya Nuh, Thamud, Lut, ikiwa ni onyo na somo kwa wanaadamu.



Virusi vya Korona vya leo huweza kuonekana kama ni onyo, mtihani au hata adhabu ya Mwenyezi Mungu (swt). Hivyo, kirusi, ambacho kinaleta magonjwa au kifo kwa mtu binafsi, ni maafa kwa mtu binafsi. Kwa upande mwengine, hatua zisizofaa na maamuzi mabaya kama kuwafungia watu yanayo chukuliwa na serikali kutokana na virusi hivi, ambayo yanawasukuma watu na jamii katika ugumu wa maisha na kuvuruga akili za watu na jamii pamoja, ni maafa ya kiwango cha kijamii. Swala za pamoja (katika kila dini), kuhudhuria mazishi, kuzuru wagonjwa, kukusanyika kwa ajili ya uzawa wa mtoto na harusi ni mahitaji yenye umuhimu, ni ya lazima kwa kila jamii. Kuwanyima watu haya ni maafa ya upande wa kijamii, ambayo yanawakumba sio tu Ummah lakini pia wanaadamu wote.

Tunashuhudia kuwa madhara yaliotarajiwa ya COVID-19 kwa kiasi kikubwa hayajafikia madhara yaletwayo na serikali zisizo na huruma na za kipumbavu, zinazotumia virusi kwa mipango yao wenyewe. Kiwango cha vifo hakijawa kikubwa kama walivyokadiria, na hospitali hazikuzidi uwezo wake. Idadi ya walio athiriwa na virusi ni kubwa zaidi kwa mamia ya idadi ya waliopata ugonjwa. Idadi ya vifo ni fungu la elfu tu ya idadi iliotarajiwa. Hivyo, maafa halisi yameongezwa na kukuzwa kwa kasi ya kikatili kwa wanaadamu na nguvu za wakoloni mabepari kote duniani. Kwa usahihi zaidi, maafa ya kikweli ni wanaadamu kunyimwa mfumo wa uadilifu, huruma na baraka wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Japokuwa Waislamu wanaihisi misiba hii zaidi ya wanaadamu wengine, kwao ni mitihani tu, ambayo hupelekea mafanikio katika dunia hii na Akhera. Hata hivyo, athari ya maafa haya itabaki juu ya makafiri hapa duniani na Akhera. Hivyo maafa yanayo wakumba Waislamu, kwa wanaadamu wengine ni mabaya kwa mara nyingi zaidi. Mwanachuoni mkubwa Ibn Qayyim Al-Jawziyya amesema, “Msiba juu ya Muumini, ni mwepesi zaidi kuliko msiba juu ya kafiri”.

Kwa zaidi ya karne moja sasa, Waislamu na wanaadamu wote, wanahangaika wakiwa chini ya unyonyaji, vita, uvamizi na aina zote za dhulma na mabalaa yanayo wakumba kutoka kwa dola za kikafiri za kikoloni, kwa sababu tu Ummah wa Kiislamu umepoteza ngao ya kujihifadhi wenyewe na walimwengu dhidi ya aina zote za maafa. Kuvunjwa kwa Khilafah katika mgongo wa sayari hii ni maafa makubwa zaidi kwa wote, Ummah na wanaadamu wengine.




Ni kutokana na haya, Ummah wa Kiislamu, (ambao ni) mwenge wa walimwengu, hauwezi kujihifadhi wenyewe na wanaadamu kutokana na kiza. Kwa hakika, Mtume (saw) ametujulisha sisi kuhusu kuja kwa masiku haya:

«لَيُنْقَضَنَّ عُرَى الْإِسْلَامِ عُرْوَةً عُرْوَةً فَكُلَّمَا انْتَقَضَتْ عُرْوَةٌ تَشَبَّثَ النَّاسُ بِالَّتِي تَلِيهَا وَأَوَّلُهُن نَقْضًا الْحُكْمُ وَآخِرُهُنَّ الصَّلَاةُ»

**"Mafundo ya Uislamu yatafumuliwa moja baada ya moja, kila linapofunguliwa fundo moja watu watashikilia lile linalofuatia, la mwanzo kufumuliwa ni utawala na la mwisho wao ni swala." (Hakim, Ahmad)**

Kwa hiyo fundo la mwanzo, nidhamu yetu ya kisiasa limeshafumuliwa, likiiacha Dini yetu na sisi, wanajumuiya wake, bila ya ulinzi, ikitupora Khalifah wetu, ngao yetu. Zaidi ya hayo, muda wote katika miezi michache iliopita, tumeporwa swala zetu kwa kisingizio cha kirusi kidogo… Bila shaka, tunaendeleza swala zetu za mtu mmoja mmoja, lakini tumekosa swala za jamaa, swala zetu katika muundo wa mujtamaa mzima wa Waislamu! Wametupora swala zetu Ijumaa, swala za Taraweh na swala za Idd!!!

Imam Ghazali (rh) amesema katika kitabu chake, Al-Iqtisad Fi'l-Itiqad: "Dini na Dola ni mapacha. Hivyo dini ni msingi na mtawala ni mlinzi: kile ambacho hakina msingi huvunjika na kile ambacho hakina mlinzi hupotea." Hii inamaana kuwa wakati wowote pindi dini ya Uislamu na utawala wa Uislamu vinapotenganishwa, Ummah wa Kiislamu na wanaadamu wote, wanabaki bila ulinzi na kuwa katika mazingira magumu. Kwa hakika, ni wazi kwa kila Muislamu mwenye akili timamu na wasio Waislamu hivi leo kuwa kipote cha watandawazi hutaka kupunguza idadi ya watu duniani. Kote katika ulimwengu wa nchi tajiri za kirasilimali zikiwemo Amerika, Uingereza, Ujerumani na nchi nyingi

nyengine za Ulaya watu wanalalamika dhidi ya kunyimwa uhuru wao, demokrasia na hata katiba, ambavyo walifanywa waviamini hadi leo.




Hata hivyo, malalamiko yao yananyamazishwa na polisi. Machafuko haya, ambayo yanaongezeka kote duniani, hayaonyeshwi au yanaonyeshwa kwa namna ya kupotoshwa na vyombo vikuu vya habari, ambavyo ni ala za serikali zinazotawala.

Kitendo na mwitiko wa mtu binafsi kwa maafa ni katika namna ya kumuomba Mola wake kwa dua na swala, na kuonyesha subira, kwa kuwa hivi ndivyo Mola wetu anatutaka tufanye:

[يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱسْتَعِينُواْ بِٱلصَّبْرِ وَٱلص◌ّلَوٰةِ◌ إِنَّ ٱللَّهَ مَعَ ٱلصَّٰبِرِينَ]

**"Enyi mlio amini! takeni msaada kwa subira na swala. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanao subiri." (Al-Baqara: 153)**

Lakini hili sio tendo la kijamii na mwitiko kwa maafa! Subira, dua na kuomba kwa jamii viko katika muundo wa "kuamrisha mema na kukataza maovu" kwa watawala. Subira (kwa upande wa) jamii ni kuwalingania watawala kukataa mifumo ya kikafiri na badala yake kutawala kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu! Mwitiko wa jamii kwa maafa ni kupitia kufanya bidii kubadilisha kile ambacho kina madhara na kinacho sababisha dosari ndani yake chenyewe. Mapambano haya ni faradhi juu ya mujtamaa wa Waislamu na ndio taji la faradhi zote! Pindi Mwenyezi Mungu (swt) anaposema katika Sura Ar-Ra'd 11,

[إِنَّ ٱللَّهَ لَا يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتَّىٰ يُغَيِّرُواْ مَا بِأَنفُسِهِمْ]

**"Hakika Mwenyezi Mungu habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo nafsini mwao."**




Yeye (swt) ameitaka jamii ya Waislamu kujibadilisha yenyewe. Hivyo, maadamu mujtamaa wa Waislamu haujaondoa sababu za machafuko ndani yake yenyewe, Mwenyezi Mungu (swt) hatoondoa maafa kwake, na hautoweza kuwa muokozi wa wanaadamu.

Enyi Waislamu! Ni Uislamu, ambao utafukuza aina zote za maafa! Ni Uislamu, ambao unatibu aina zote za maradhi, na kumaliza mauwaji, uvamizi, ufukara, kutojiweza, uoga, upweke, ulegevu, uhaini nk.! Ummah huu unabeba maagizo pamoja na dawa dhidi ya uchoyo na watawala wasio na huruma ambao wanatumikia maslahi ya kipote cha mabepari! Uislamu ndio nguvu pekee, ndio mkono pekee, ndio ngumi pekee iwezayo kuwaokoa wanaadamu kutokana na fumbato la ujinga na ukafiri!

[ٱلْحَقُّ مِن رَّبِّكَ فَلَا تَكُونَنَّ مِنَ ٱلْمُمْتَرِينَ]

**“Haki inatoka kwa Mola wako Mlezi. Basi usiwe miongoni mwa wanaofanya shaka” (Al-Baqara: 147)**

Zehra Malik

# MASHIRIKA YA KIMATAIFA HAYAPASWI KULAUMIWA KWA AFYA YA ULIMWENGU




Trump alisema katika mkutano wake wa kila siku na waandishi wa habari mnamo 10 Aprili 2020 kuwa, "Kwa kipindi cha miaka yote, miaka mingi, tumekuwa tukiwalipa kwa kiasi cha dolari milioni 300 hata 500, na hata zaidi, kwa mwaka. China imekuwa akiwalipa chini ya 40 kwa miaka yote hiyo. Hivyo tunawalipa mara 10 zaidi ya China. Na wao, wangali wamepagawishwa mno na China."

Shambulizi la Trump kwa juhudi za Shirika la Afya Duniani (WHO) za kukabiliana na janga hili limechipuza kutokana na hamu ya kutaka kujipurukusha kutokana na kushinda kwake yeye mwenyewe katika kukabiliana na janga hili, na inaonyesha dosari halisi katika muundo na utendakazi wa mashirika ya kimataifa chini ya mwavuli wa Umoja wa Mataifa na inaungwa mkono kwa kiasi fulani kwa makosa halisi yanayo fanywa na Shirika hilo la Afya Duniani.

Mnamo 14 Januari Shirika la Afya duniani WHO liliandika kwenye mtandao wake wa tweeter kwamba "Uchunguzi wa awali uliofanywa na mamlaka za China umekuta kwamba hakuna ushahidi wa wazi wa maambukizi kati ya mtu na mtu ya virusi vya korona vilivyo gunduliwa jijini Wuhan, China", lakini madaktari wa China walikuwa wanajaribu kuionya dunia mapema kabisa tangu Disemba kwamba maambukizi kati mtu na mtu yalikuwa yakitokea. Kuongezea mkanganyiko huu kutoka Shirika la Afya, WHO ilichelewa sana kutangaza kuwepo kwa janga la virusi na hili likazipa serikali za kitaifa uhalali wa kirongo wa kuchelewa kwao kuchukua hatua.

WHO inazingatiwa kwa kiasi kikubwa kuwa ni taasisi huru, lakini, bila shaka, Trump yupo sahihi kwamba shirika hilo limeundwa na watu kutoka nchi mbalimbali kote ulimwenguni na ajenda tofauti tofauti lazima ziangaziwe katika utendakazi wa shirika hilo.



"The United Nations has increasingly become a political arena where high officials engage in political give-and-take and where 'interest groups' lobby for their country's interests [...] Political appointees are frequently not loyal to the United Nations, but to their respective governments, upon which they depend for further reward or punishment" (Finger and Hanan 1980). Increasing evidence from other domains suggests that the national identities of bureaucrats affect the decision-making of institutions (Kaja and Werker 2010; Johns 2007)

Njia kubwa inayo angazia hili, lakini, sio maamuzi yanayo unga mkono ajenda maalumu, bali ni kupitia maamuzi na matangazo yanayo penyezwa kupitia ngazi nyingi za msururu mrefu wa hatua katika jaribio la kutaka kuepukana na lawama za kidiplomasia mbele ya dola zote wanachama. Matokeo ni kwamba madai ya China lazima yayapiku madai ya Taiwan, kwani Taiwan anatambuliwa na wanachama kumi na nne pekee kati ya wanachama 193 wa Umoja wa Mataifa, na kauli rasmi za serikali ya China hutangulia (kipaumbele) juu ya madai kinzani yanayo tolewa na raia binafsi wa China. Fauka ya hayo, msururu mrefu wa hatua huhakikisha utangazaji wa polepole na wa uangalifu baada ya kujenga itifaki ya kindani ili kuepusha makosa. Kwa kuzingatia yote haya, WHO ni shirika la kibinaadamu kiasi ambacho ushawishi wa baadhi ya dola unaweza kuwa mkubwa kuliko dola nyengine kulingana na ukubwa wa dola hizi na kiwango cha uwekezaji wao. Ile fahamu ya shirika la kimataifa au sheria ya kimataifa ina dosari kwani dola pekee ndizo zinazo weza kuwa chimbuko la sheria. Dola hukubali tu kufanya kazi ndani ya hiyo inao itwa mipangilio ya kimataifa kwa mujibu wa nguvu zao na maamuzi yao juu ya iwapo mipangilio hii itatumikia maslahi yao ya muda mrefu kwa kiasi ambacho zitayatoa kafara baadhi ya maslahi ya muda mfupi.

Kwa kujua mapungufu ya kidhana na kivitendo ya WHO kama chombo cha kimataifa, uongozi wowote ulio na ikhlasi unapaswa uunde vitendo vyake juu ya msingi kuwa ni serikali za kitaifa ndio zenye kuwajibika dhidi ya afya za watu wake, na wala sio WHO. Trump, hivyo basi, anakosea kulilaumu shirika la WHO kutokana na ukweli uliopo kwamba Amerika sasa iko katikati ya janga, ambalo ukubwa wake halisi ndani ya mipaka yake unazidi uwezo wao wa kulipima.

**Dkt. Abdullah Robin**

# JE VIPI IKIWA KWELI KUNA NJAMA LAKINI SIO ILE UNAYOIFIKRIA WEWE ?




Ueneaji wa ajabu wa janga la virusi vya Covid 19 huenda kwa kweli umefananishwa na kuenea kwa ngano za vipi virusi hivi vimezuka, wapi vilianza, nani wakulaumiwa na nani anaefaidi kutokana na nchi yingi kuwekwa katika hali ya kufungiwa ndani. Uchumi wa nchi nyingi zimesimama na mtindo wa maisha wa watu umegeuzwa juu chini. Nikama inaonekana kuwa kila siku kunakuja nadharia mpya ya kufafanua vitu.

Ama kunasibisha Covid 19 na mawasiliano ya simu ya 5G kumedhaifishwa kwa kuwa hamna ushahidi wa kuaminika wa kisayansi au hoja ya kueleza kwamba kusambazwa kwa mawasiliano ya 5G yamesababisha virusi hivi kuenea au virusi hivi vinatumiwa kama finiko linalo ficha uendelezaji wa tecknologia ya 5G.

Njama za kinadharia huwepo ili kupeana maelezo ya kukabiliana au kufichua habari, zilizo fichika kwa umma juu ya matukio makubwa ya kiulimwengu. Wapo mamilioni wanaoamini kuwa kutua mwezini kwa nchi ya Marekani haikuwa ukweli.Wengi wa waisilamu huamini kuwa mayahudi walikuwa wahusika wa kuu katika tukio la 9/11. Wapo wanaodai kuwa vikosi vya usalama vya Uingereza vilikuwa nyuma ya tukio la 7/7 la ulipuzi wa mJi wa London. Mkusanyiko wa Flat Earth bado hukusanya maelfu ya watu kila mwaka wanaoamini kuwa ulimwengu upo tambarare ilhali wanaopinga chanjo hupata umaarufu kila mwaka wakati wa ujio wa upeanaji chanjo.



Sote tunayo njama nadharia tuipendayo licha ya kutowezekana kuwa ukweli: Yangu ikiwa vipi katika ulimwengu yawezekana Manchester United FC wakawa ni wenye kunyimwa ushindi dhidi ya West Ham katika masiku ya mwisho wa msimu wa mwaka wa 1994/95. Licha ya kudhibiti mchezo , kupiga mchuma na kizuizi na majaribio mengi langoni, matokeo ya mwisho yalibaki 1-1. Je wachezaji wapinzani walikuwa wamehongwa, je mpuliza kipenga alikuwa haoni vyema au mpira ulikuwa na itilafu. Hata kwa uzito wote, kutaka moja wapo wa jambo liwe la ukweli haliwezii kuwa ukweli na bila shaka utibitisho wangu ulioegemea upande mmoja kama shabiki sugu wa Man Utd uliharibu jinsi nilivyo tazama mchuwano huo.

Kwahivyo ni rahisi kuzikatalia mbali njama za kinadharia au kikosi cha' Kofia ya bati' kama inavyo julikana wakiwa katika kategori ya David leke, au kama matami kidogo yasio umiza pindi unapo kutana na mtu anaeamini Elvis bado angali yupo hai.

Mambo huanza kua magumu kidogo nyakati utaaza kubainisha kauli ilio zoeleka uhalisia wake baada ya miaka mingi kwa kupatikana maono na hoja mpya kugunduliwa. Makampuni ya tumbaku yalipiga hatua ya ajabu kueleza kuwa sigara zipo salama na kukanusha madhara ya uvutaji sigara. Mgando wa mafuta uliokuwa ndio ni wenye kunasibishwa na maradhi ya moyo na hoja ya kutabani mlo wa mafuta machahe ndio ilikuwa hoja ya kiutaalamu wa sayansi na ada ya mlo inayokubalika kwa mda mrefu. Ni majuzi tu ndio imebainika athari ya vyakula vilivyo na mjazo mwingi wa Cabohaidreti/Sukari ndio husababisha maradhi ya fetma na kisukari, na dori iliocheza ya makampuni ya kutengeza vinywaji baridi kudanganya watu kubainika. Je ni njama nadharia, au ni kula njama au ni uzemba? Pengine ni mkusanyoko wa vyote hivi.

Mtazamo wangu wa kutokubaliana na waumini wa njama nadharia ni mchache katika upande wa hoja na mwingi katika upande wa kutaka kujua ukweli uliofichika au maelezo wa mkasa wa serikali, mwanasiasa na vombo vya habari. Na hii si kwa kukana kuwa kuficha, kupeana habari isiosahihi na vitu kuelezwa tofauti na vile vilivyo ni mambo yasiofanywa-
La ila naamini mambo haya kwa kweli hufanyika.




Je vipi ikawa basi kile kinacho tafutwa ni jambo ambalo lipowazi mbele ya macho kama vile isemavyo? Je vipi ikawa mfumo tawala leo ulimwenguni, mfumo wa kirasilimali na demokrasia yake pamoja na vipimo vya vitendo vyake ndio swala nyeti lihitajio kujadiliwa?

Yeyote anaehisabu mtazamo huu wa jadi unao lingana na hali ilivyo au akawa na mtazamo tofauti hutambulika kuwa yeye si mwanahuria.

Misingi ya miito ya uhuru asili haikaguliwi au haiekwi kwa mizani na jamii kwa kawaida. Huwa ni yenye kudhaniwa eti ndio kipimo ambacho kila kitu hugemezwa kwake bila kuhojiwa. Mfano ni nidhamu ya kisiasa ya Uingereza, je wananchi ni wenye kuchaguwa philosofia wanayoishi chini yake na msingi wa vipi sharia inavotengenezwa? La asha. Wala haija kuwa kura ya maamuzi ilio na swali la kuchaguliwa kati ya maono haya: urasilimali, ukomonisti au uisilamu? Wala jambo hilo halitowezekana kamwe.

Sote hadi sasa twafahamu kupitia televisheni jinsi muelekeo kila siku ulivyo juu ya vifo vya Covid 19, walioambukizwa na waliolazwa mahospitalini. Zipo chati zinazo onyesha vifo vya kila siku, mateso, umasikini na ufukara unaokumba mamilioni ya watu ulimwenguni wakiwa niwenye kustirika na dolari moja kwa siku. Janga hili la Covid 19 litapungua lakini lile litakalo baki halibadiliki ni mfumo wa kimaisha wa klimagharibi na mitaazame yake ya uhuria ulimwenguni ambayo tangu mwanzoni yamechangia pakubwa kuangamiza hali ya kibinaadamu.Na hatari zaidi ni kuwa bado hatutalizungumzia hili nyakati ambao yastahiki hili lijadiliwe. Na hii ndio njama nadharia.

**Imeandikwa na Mwanachama wa Hizb ut Tahrir**.

# RAMADHANI NYENGINE IMEINGIA BILA YA KHILAFAH



Enyi Waisilamu,! wacheni ikuwe hii ndi Ramadhani ya mwisho tulio nayo bila Khilafah.

Sifa ni za Allah وتعالى سبحانه amabare ndie alietusuhudishia sisi Ramadhan amabayo mwanzo wake ni rehma, kati yake ni usamehevu na mwisho wake nikuhifadhiwa na moto wa Jahanam. Ni miezi tisaini na sita ya Ramadhani imepita kwa sasa bila ya Khalifah na Khilafah . Na sasa twaiyaga tena na bado tumegawanyika. Umma ya kiisilamu tangu kuanguka kwa Khilafah mwakani 1342 H haijawahi kufunga swaum ya Ramadhani ndani ya masiku ma mmoja. Nyakati tulipokuwa na Khilafah, tuliwahi kufunga siku mmoja na kusheherekea Idd siku moja.Tangu siku hiyo tumekuwa tukitumbukia kwa janga mmoja hadi jengine huku tukiwa ni wenye kugawanywa, kutapakanywa na kupoteza nguvu yetu kwa kuwa tumepoteza serikali yetu.

Idadi yetu ulimwenguni imepita bilioni lakini hata hivyo bado ni kama mapovu ya baharini. Kauli ya Mtume wetu عليه الله صلى وسلم kwa uhakika ya shibiana na uhalisia wa maisha yetu: «يُوشِكُ أَنْ تَدَاعَى عَلَيْكُمْ الْأُمَمُ مِنْ كُلِّ
أُفُقٍ كَمَا تَدَاعَى الْأَكَلَةُ عَلَى قَصْعَتِهَا»، قَالَ: قُلْنَا: يَا رَسُولَ
اللَّهِ، أَمِنْ قِلَّةٍ بِنَا يَوْمَئِذٍ؟ قَالَ: «أَنْتُمْ يَوْمَئِذٍ كَثِيرٌ، وَلَكِنْ
تَكُونُونَ غُثَاءً كَغُثَاءِ السَّيْلِ، يَنْتَزِعُ الْمَهَابَةَ مِنْ قُلُوبِ
عَدُوِّكُمْ، وَيَجْعَلُ فِي قُلُوبِكُمْ الْوَهْنَ»، قَالَ: قُلْنَا: وَمَا
الْوَهْنُ؟ قَالَ: «حُبُّ الْحَيَاةِ، وَكَرَاهِيَةُ الْمَوْتِ»

**“Watu karibuni watakuwa ni wenye kuitana kwa minajili ya kuwavamia nyie, kama vile wanavyoitana pindi watakapo kuwa ni wenye kula. Mmoja akauliza:Jr ni kuwa tutakuwa ni wachache nyakati hizo? Akajibu: La mutakuwa wengi nyakati hizo lakini mutakuwa kama povu la baharini na Mola swa ataondoa hofu juu yenu kwenye vifua za maadui wenu na ataweka wahn katika nyoyo zenu.” Mmoja akauliza, “Ni nini wahn? Mtume wa Mwenyezi Mungu saw akajibu,”Ni kupenda dunia na kuchukia mauti.” [Ahmad Bin Hanbal]**



Hivi ndivyo jinsi ya vipi makruseda wakiongozwa na Amerika na Uigereza walivyo jikusanya na kuvamia ardhi za waisilamu. Wamekalia kimabavu ardhi tukufu ya Palastina na kuwauwa vijana wake, walikanyaga nyayo zao katika sehemu zilizo tukufu na kisha kunyakuwa na kupora mali zao: lakusikitisha zaidi fauka ya haya ni kuwa bado viongozi wa biladi za kiisilamu wanaendelea kutabikisha sera za wakoloni hao wamagharibi. Viongozi hawa wamekuwa wafanya kazi kuzima mapinduzi dhidi ya tawala dhalimu na kusaliti waisilamu damu zao nchini Syria na Iraqi.

Enyi waisilamu! Mumefahamu  Ramadhani ni mwezi wa Quran na Ramadhani ni mwezi wa huruma, usamehemu na baraka pamoja na kukingwa na moto, hivyo basi lazima tuzidishe amali zetu za ziada na tuelekee kuomba msamaha na kutafuta kusamehewa na kusujudu kwa usawa.Pia mumeafamu kuwa Ramadhani ni mwezi wa Jihadi na ufunguzi na kusimaisha Khilafa Rashidina ni uwajibu mkubwa ambao kwayo wajibu zengine hutegemea.

Ama Khilafah ndio mama wa faradhi zote amabayo kwake pekee bendera ya Jihadi husimamishwa na kwake pekee maisha, heshima na mali huhifadhiwa. Ni kwake pekee waisilamu huregelea izza, hadhi na heshima yao ya kale.Basi ni lazima tukimbilie kusimamisha tena Khilfah takatifu kabla mwezi mwengine takatifu wa Ramadhani kutuingililia na hii ni bila kuhofia lawama za wenye kulaumu.




Enyi waisilamu, tumengoja vya kutosha, illa sasa ni wakati wa kufanya kazi kuiregesha tena Khilafah. Kwahivyo tujityolee ili hii iwe ni Ramadhani ya mwisho ilo pita bila Khilafah na ili iregee Ramadhan kama ilivyokuwa: Mwezi wa ushindi na ukombozi: na swala hili ni sahali kwa Allah وتعالى سبحانه.

Katika mwezi tukufu huu wa Shawaal, twapenda kuwatakia nyie na umma jumla Ramadhani ilio kubaliwa ya Baraka na twamuomba Mola [swa}ajaalie miezi inayo kuja iwe yaushidi kwa kuregesha tena Khilafah Rashidina.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اسْتَجِيبُواْ لِلّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُم لِمَا يُحْيِيكُمْ وَاعْلَمُواْ أَنَّ اللّهَ يَحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ وَأَنَّهُ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ

“ Enyi mulio amini, itikieni mwito wa Allah na Mtume wake pindi wanapo kuiteni kwa yale ambayo ni yenye kupeana uhai.Na jueni ya kwamba Mola huingilia kati baina ya mja na moyo wake na kwake Yeye mutakusanywa.” (Al-Anfal: 24)

**Imeandikwa na Mwanachama wa Hizb ut Tahrir.**

# Jarida la UQAB



uqab.or.ke
uqab_htk
UQAB-Magazine-1911964012162253